- Kiasi cha salfa kinachopendekezwa ni kati ya gramu 125 na 250 kutegemea ukubwa wa mkorosho.
- Inapendekezwa mpulizo wa kwanza uanze pale ambapo asilimia 20 ya maua yameshajitokeza na zaidi ya asilimia 5 yanaonesha dalili ya ugonjwa.
- Inapendekezwa mpulizo wa kwanza uanze pale ambapo asilimia 20 ya maua yameshajitokeza na zaidi ya asilimia 5 yanaonesha dalili ya ugonjwa.
- Inapendekezwa upuliziaji ufanyike mapema asubuhi ambapo majani na maua yana umande
- Pulizia salfa kwa kila baada ya siku 14 kwa awamu tatu za mwanzo ikifuatiwa na siku 21 kwa awamu mbili za mwisho

(Siku 14 →14 →14 → 21→21)

Viuatilifu vingine

- Tumia viuatilifu vyenye kemikali zifuatazo ndani yake (Tridimenol na Hexaconazole) ili kudhibiti ugonjwa huu
- Changanya mililita 15 za viuatilifu hivyo ndani ya lita moja ya maji.
- Pulizia kiuatilifu kila baada ya siku 21



## 6.0 Kuchanganya mipulizo ya viuatilifu

- Changanya mipulizo ya viuatilifu kama ifuatavyo:
  i. Tumia viuatilifu vilivyo katika hali ya maji vya kudhibiti Ubwiri unga na wadudu waharibifu katika mpulizo wa kwanza
  ii. Baada ya siku 21 tumia Salfa
  iii. Baada ya siku 14 rudia kupulizia viuatilifu vilivyo katika hali ya maji vya kudhibiti Ubwiri unga na Wadudu
  iv. Baada ya siku 21 pulizia tena Salfa
  v. Baada ya siku 14 rudia kupulizia viuatilifu vilivyo katika hali ya maji vya kudhibiti Ubwiri unga na Wadudu

TARI
Transforming Agriculture

# UJUE UGONJWA WA UBWIRI UNGA WA MIKOROSHO



*Kimetayarishwa na:*
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz

April 2019

# UGONJWA WA UBWIRI UNGA.

## 1.0 Utangulizi

Moja ya matatizo makubwa ya uzalishaji wa zao la korosho ni ugonjwa wa Ubwiri unga, ambao umeenea katika mikoa yote Tanzania. Ugonjwa huo husababishwa na vimelea aina ya kuvu na huweza kupunguza mavuno kwa zaidi ya asilimia 70.

## 2.0 Mashambulizi ya Ubwiri unga

- Hushambulia sehemu teketeke (majani, maua, mabibo na korosho changa) katika mkorosho.
- Husababisha maua kushindwa kufunguka kuchavushwa hatimaye kunyauka na kukauka.

## 3.0 Dalili za ugonjwa

Kuonekana kwa unga unga mweupe au/ na kijivu uliofunika sehemu teketeke za mkorosho



*Dalili za Ubwili unga kwenye majani*

- Majani yaliyoshambuliwa husinyaa, hubadilika rangi, wakati mwingine hukunjamana.
- Majani machanga zaidi yanaweza kupukutika.
- Majani machanga yaliyoshambuliwa yanapokomaa huwa na mabaka ya rangi ya kahawia.
- Maua yaliyoshambuliwa sana hushindwa kuchanua na hatimaye hukauka kabisa na kuwa rangi ya kahawia.



Mabibo yaliyoshambuliwa hudumaa, huwa na mipasuko na hupoteza rangi yake.

- Korosho changa zilizoshambuliwa huweza kubadilika rangi na kupukutika.
- Korosho zilizoshambuliwa zikifikia kukomaa, hupoteza rangi ya kijivu na hutengwa katika daraja la pili.



*Athaliza Ubwili unga kwenye bibo na tegu*

## 4.0 Kuenea kwa ugonjwa

- Vimelea vya Ubwiri unga vinaishi kwenye mimea iliyo hai tu.
- Ugonjwa huu hushamiri katika majira yenye ukungu, hususan kuanzia mwezi Mei/Juni hadi Septemba na husambazwa kwa upepo
- Ugonjwa huo hushamiri zaidi kipindi cha nyuzi joto kuanzia 26 hadi 28 za Sentigredi na unyevu hewani kuanzia asilimia 80 hadi 100
- Ubwiri unga hupendelea zaidi mikorosho iliyosongamana
- Katika kipindi cha Oktoba hadi Aprili vimelea hujificha na kuishi kwenye maotea au machipukizi ambavyo baadaye huwa ni chanzo cha Ubwiri Unga

## 5.0 Kudhibiti Ubwiri unga.

Kuna njia tatu zinazotumika kudhibiti Ubwiri unga

### 5.1 Udhibiti sango

- Kuondoa machipukizi na maotea ili kupunguza kasi ya kuenea ugonjwa wa Ubwiri Unga
- Kupogolea matawi ya mikorosho ili kuruhusu mzunguko wa hewa
- Ng'oa mikorosho iliyosongamana kwa kuzingatia uzaaji ili kuruhusu mzunguko wa hewa shambani.

### 5.2 Matumizi ya mbegu bora

- Panda mbegu bora zinazovumilia mashambulizi ya ugonjwa wa Ubwiri unga

### 5.3 Matumizi ya viuatilifu

**Salfa**

- Salfa ni kiuatilifu katika hali ya unga
- Hupulizwa kwa kutumia mashine